# Rais Dk. Mwinyi ataja mikakati kuinua wavuvi Zanzibar, Bara

**Na MWANDISHI WETU,** *Zanzibar*

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk.Hussen Ali Mwinyi, amesema serikali zote mbili zitaendelea kutekeleza kikamilifu dira, mipango ya maendeleo na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025.

Pia, serikali hizo mbili zitaendelea kutekeleza sera na mikakati ya maendeleo endelevu ya sekta ya uvuvi nchini ichangie pato la taifa.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Makamu wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, kwa niaba ya Rais Dk.Mwinyi,katika Maadhimisho ya Siku ya Uvuvi Duniani, iliyofanyika katika Ukumbi wa Golden Tulip, Zanzibar.

Dk. Mwinyi alisema katika kukuza na kuimarisha mnyororo wa thamani katika sekta ya uvuvi na mazao ya baharini, serikali itaendelea kupiga vita uvuvi haramu na kuvitaka vyombo husika kuendelea kuchukua hatua stahiki kupiga vita vitendo hivyo.

Alisema kuwepo kwa siku ya uvuvi duniani kunatokana na Tamko la Umoja wa Mataifa la kushajihisha uvuvi endelevu wenye tija kwa wananchi, hivyo serikali zitaendelea kuwawezesha wavuvi kwa kuwapatia elimu, nyenzo, mitaji na masoko kujipatia ajira na kipato kinachokidhi mahitaji.

Rais Dk. Mwinyi alisema serikali itaendelea kuwapatia vyombo na nyenzo za kisasa, zitakazowawezesha kuingia katika uvuvi wa bahari kuu, kuwawekea miundombinu iliyo bora, ikiwemo ujenzi wa madiko ya kisasa, masoko na mitambo ya kuhifadhia samaki.

Alisema katika kuhakikisha sekta ya uvuvi inafanikiwa zaidi, serikali zimejipanga kujenga viwanda vya kusarifu na kuchakata minofu ya samaki, dagaa na kuwekeza zaidi kwa kuwawezesha wavuvi kufuga na kuzalisha samaki katika bahari na maji baridi.

Kwa mujibu wa Dk. Mwinyi, kupitia programu ya Ahuweni ya Uviko-19 ya Uchumi wa Buluu kwa Zanzibar, ambapo boti 577 za uvuvi zimetolewa, boti 500 wamepatiwa wakulima wa mwani.

Alifafanua, pia,vilitolewa vifaa vya uvuvi kama vile mishipi, nyavu, GPS na 'fish finders,'kamba na tai tai kwa wakulima wa mwani na kujengwa kiwanda cha kisasa cha kusarifia Mwani.

**ULEGA**

Kwa upande wake, Waziri wa Mifugo na Uvuvi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Abdallah Ulega, alisema wizara zote mbili zitatoa fursa sawa kwa wavuvi wa pande zote mbili, kwa kuwapatia vitendea kazi kuwezesha uvuvi wa kisasa.

Alisema kwa Tanzania Bara, zaidi ya wavuvi 197,000 tayari wameshapatiwa leseni za uvuvi wa Bahari Kuu, kupatiwa zana zote ambazo zitawasaidia kuvua kisasa na kukuza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa.

**WFP**

Mkurugenzi Mkazi kutoka Shirika la Chakula Duniani (WFP),Sara Golden Gipson, alisema WFP imekuwa ikichangia katika shughuli za maendeleo ya uchumi wa Zanzibar, hasa katika sekta ya uvuvi na kuwanyanyua wanawake kiuchumi kwa kuwajengea uwezo kwa kuwapatia miradi ya maendeleo.

Sara alisema WFP imekuwa ikiwasaidia wanawake kuhakikisha wanapiga hatua za maendeleo, kwa kuwatatulia changamoto zinazowakabili katika shughuli zao kama vile uhaba wa vitendea kazi hasa kwa wakulima wa mwani na kuwapatia maboksi ya kuhifadhia samaki kwa muda refu.

**197,000>Ni wavuvi waliopewa leseni za uvuvi wa Bahari Kuu Bara**

POLE